

Tumefungua Bima ya Afya kwa **Kila Mtu!**

MPYA! Kununua bima ya afya imekuwa rahisi kwa wahamiaji wasio na vibali.

Kuanzia mwezi huu wa Novemba, kila mtu anayeishi katika jimbo la Washington atakuwa na uwezo wa kununua bima ya afya na meno kupitia *Washington Healthplanfinder*, bila kujali hali yake ya uhamiaji.

Kila mtu anaweza kujiandikisha kuanzia Novemba 1, 2023.

Jisajili ifikapo Desemba 15 kwa bima ya afya inayoanza Januari 1, 2024. Kipindi cha kujiandikisha kinaisha Januari 15, 2024.



Pata msaada kuhusu malipo yako ya kila mwezi ya bima

Punguzo kwa wenye kipato kidogo

Unaweza kufuzu Cascade Care Savings, jambo linalomaanisha jimbo la Washington litalipa sehemu ya bima yako ya afya. Kipato cha kaya yako kikiwa na vigezo vya hapo chini, unaweza kufuzu.

\$36,450	\$49,300	\$62,150	\$75,000	\$87,850	\$100,700
Mtu mmoja	Familia ya watu 2	Familia ya watu 3	Familia ya watu 4	Familia ya watu 5	Familia ya watu 6

Usalama wako ni muhimu kwetu.



- Kujiandikisha **hakuathiri** hali yako ya uhamiaji au maombi ya uraia kwa ajili yako, familia yako, au yeyote anayeishi pamoja nawe.
- Sheria za serikali kuu na za jimbo zinalinda faragha ya watu wanaotuma maombi ya bima ya afya kupitia *Washington Healthplanfinder*. Taarifa kuhusu hali ya uhamiaji zitatumika tu kubaini ustahiki wa kupata bima na si kwa ajili ya ushurutishaji wa uhamiaji.

Unahitaji msaada? Njia 3 za kupata usaidizi wa **BURE wa kujiandikisha**

Piga

Kituo cha Usaizi kwa Wateja

Nambari ya Bure:

1-855-923-4633

TTY/TDD: 1-855-627-9604

Saa: 7:30 am hadi 5:30 pm
Msaada unapatikana kwa lugha zaidi ya 200.

Tembelea

Tovuti yetu

wahealthplanfinder.org



au tambaza msimbo wa QR kupitia kamera yako

Wasiliana

Kupitia mtaalamu mahalia*

Wasiliana nami Novemba 1 kujiandikisha!

*Navigator na Broker wanaweza kukusaidia kuelewa msaada wa kifedha unaopatikana, kujibu maswali kuhusu bima ya afya, na kukusaidia kununua bima. Ikiwa hujui iwapo mtu fulani ameidhinishwa kukupa usaidizi, wapigie Kituo cha Usaizi, wapigie Kituo cha Msaada kwa Wateja cha Washington Healthplanfinder kupitia 1-855-923-4633.

